

TANZANIA LAYERS FARMERS ASSOCIATION



Vision

Kuwa chama bora chenye mafanikio katika tasnia ya kuku wa mayai Tanzania.

Mission

Kuwaunganisha wafugaji wote wa kuku wa mayai Tanzania kwa kuwapatia jukwaa la kutetea haki zao, elimu sahihi ya ufugaji wa kuku na kuunda mtandao wa masoko ya uhakika kwa mazao ya kuku wa mayai.

Malengo ya Makuu ya chama

- Kuwa jukwaa kwa chama cha Tanzania Layers Farmers Association. Kuibua maswala, kujadili na kutafuta ufumbuzi wa pamoja kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine muhimu.
- Kuanzisha na kudumisha taasisi katika Tanzania kwa ajili ya kukuza maendeleo na mwongozo wa biashara katika sekta ya mayai kama taasisi tanzu inayojitegemea katika tawi la chama cha Poultry Association of Tanzania (PAT) kwa kuwa na hadhi sawa kama zinazopewa tanzu nyingine ambazo ni matawi ya sekta ya kuku.
- Kuwa nguvu ya pamoja kwa ajili ya kujadiliana, kuzungumza, kuanzisha, kuchunguza na kutoa ushauri kwa maswala makubwa yanayogusa maslahi ya wanachama kwa pamoja au mmoja mmoja
- Kuwakilisha wanachama katika majadiliano na serikali, na umma na taasisi zisizo za kiserikali kwa maslahi mapana ya wanachama.
- kuwaelimisha wafugaji wa kuku wa mayai njia za kisasa za ufugaji wa kuku kwa kutengeneza mazingira mazuri. Kuhamasisha elimu ya

ufugaji kwa kufanya au kusaidia katika uchunguzi wenye asili ya kinadharia na kisayansi na kuandaa warsha kwa kuanzisha na kuongeza utamaduni wa kujifunza miongoni mwa wanachama wa TALFA.

- Kujenga uhusiano na watunga sera, mashamba mama ya kuku wazazi, watengenezaji wa chakula, wasindikaji wa bidhaa za kuku na masoko kwa lengo la kuongeza uzalishaji wenye tija.
- Kuhakiki kwa umakini usalama wa kuku na mazao kwa kutembelea mifugo ya wanachama.
- Kulinda haki ya walaji dhidi ya bidhaa dhaifu za kuku na mazao yake
- Kuhamasisha utafiti na maendeleo ya mfumo wa uzalishaji wa kuku ndani ya nchi miongoni ya mwanachama
- Kuratibu ushirikiano na mashirika mengine ya kimataifa katika kuleta maendeleo ya sekta ya kuku kwa faida ya wanachama
- Kuwezesha, kushawishi na kuwasiliana na serikali na wakala wa serikali kuhusu ubora na hatma ya kuendeleza wafugaji wadogo na wakulima kwa kuwahakikishia ufanisi unaofaa katika hali ya utoaji wa msaada katika kila eneo
- Kukusanya taarifa za soko na kuzifanya zipatikane kwa wanachama wote wa TALFA kwa kuwasaidia kufanikisha bidhaa zao sokoni na uelewa wa ugavi kwa ujumla.
- Kuwa na mikakati ya maendeleo ya soko itakayoleta tija kwa wanachama wa TALFA

Jinsi ya kujiunga na TALFA

- mwanachama mwombaji anatakiwa kuomba kujiunga na umoja bila kulazimishwa Kujiunga na kwa hiari yake mwenyewe.
- Mwanachama mwombaji atatakiwa kujaza Fomu maalumu.
- Mwanachama atakayeomba atawajibika kulipia Kiingilio na ada ya mwaka iliyokubaliwa na kupitishwa na Mkutano mkuu.

Mawasiliano

+255 753 469 241/715691863